

**TAARIFA KWA UMMA****MATUMIZI YA MFUMO WA eMREJESHO KUTUMA
MALALAMIKO, MAPENDEKEZO, MAULIZO AU PONGEZA KWA
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI (LATRA)**

Dar es Salaam,

Tarehe 30, Septemba, 2023.

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inawataarifu wananchi na umma kwa ujumla kuwa imeanza rasmi kutumia mfumo wa eMrejesho kwa ajili ya kupokea malalamiko, mapendekezo, pongezi au maulizo. Hivyo, wananchi wote mnashauriwa kutumia mfumo huo unaopatikana kwa anwani ya <https://emrejesho.gov.go.tz/> au kwa kupakua Mobile App ya eMrejesho au kwa kutumia simu yako kwa njia ya Msimbo (USSD) au kwa kupitia tovuti ya Mamlaka <https://www.latra.go.tz/> sehemu ya tovuti mashuhuri.

Kutuma malalamiko kwa kutumia tovuti, fuata maelekezo yafuatayo;

- a. Andika <https://emrejesho.gov.go.tz/> kwenye browser kisha
- b. Andika neno LATRA sehemu ya kulia ilioandikwa Tafuta Taasisi
- c. Bofya neno Fungua kwenye Taasisi ya LATRA
- d. Bofya neno Mwananchi
- e. Chagua namna ya kutuma Lalamiko, Pendekozo, Pongezi au Maulizo yako
- f. Chagua kupitia kufungua akaunti yako, kwa kuweka taarifa zako au kwa kutuma bila kujulikana
- g. Jaza Fomu ya Taarifa za Lalamiko, Pendekozo, Pongezi au Maulizo
- h. Bofya neno endelea, kisha
- i. Bofya neno tuma

Kutuma malalamiko kwa kutumia Mobile APP, fuata maelekezo yafuatayo;

- a. Pakua App ya eMrejesho kwa simu za Android (kwenye Play Store) au IOS (kwenye App Store)
- b. Andika neno LATRA sehemu Tafuta Taasisi
- c. Bofya neno tuma
- d. Chagua tuma kama mwananchi
- e. Chagua namna ya utumaji (Bila kujulikana, kupitia akaunti yangu au weka taarifa zangu), kisha bofya neno endelea
- f. Jaza fomu ya taarifa za malalamiko, maulizo, mapendekezo au pongezi
- g. Kisha bofya neno tuma

Kutuma malalamiko kwa simu kupitia Msimbo, fuata utaratibu ufuatao;

- a. Andika namba *152*00#
- b. Kisha chagua namba 9 (Malalamiko, Sheria, haki)
- c. Kisha bofya namba 2 (eMrejesho)
- d. Kisha chagua aina ya taarifa unayotaka kutuma (tuma lalamiko, pendekero, pongezi, tuma maoni, fuatilia lalamiko au kata rufaa ya lalamiko)
- e. Weka jina lako
- f. Andika jina la Taasisi kwa ufupi- LATRA
- g. Andika lalamiko lako

Ili kufahamu kama taarifa yako imefanyiwa kazi,

- a. Utapata ujumbe mfupi kupitia simu yako ya mkononi endapo ultumia akaunti yako ya eMrejesho / ulijaza taarifa zako / Msimbo
- b. Tumia, namba ya utambulisho (ID) ya taarifa yako kupitia tovuti ya eMrejesho, Mobile App au Msimbo.

Imetolewa;

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano